THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA
NATIONAL EXAMINATIONS COUNCIL
ADVANCED CERTIFICATE OF SECONDARY EDUCATION EXAMINATION

121/1 **KISWAHILI 1**
(Kwa Watahiniwa Walioko Shuleni tu)

**Muda: Saa 3** **Jumatatu, 07 Februari 2011 asubuhi**

## MAELEKEZO

1. Karatasi hii ina maswali **kumi na tatu** (13) katika sehemu A, B, C, D na E.
2. Jibu maswali **matano (5)** kwa kuchagua swali **moja (1)** kutoka kila sehemu.
3. Kila swali lina alama **ishirini (20).**
4. Simu za mkononi **haziruhusiwi** katika chumba cha mtihani.
5. Vikokotozi **haviruhusiwi** katika chumba cha Mtihani.
6. Andika **Namba yako ya Mtihani** katika kila ukurasa wa kijitabu chako cha kujibia.

Karatasi hii ina kurasa 4 zenye maandishi.

Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

## SEHEMU A (alama 20)

## HISTORIA YA KISWAHILI

1. "Ingawa wazungu ndio watu wa kwanza kukisanifisha Kiswahili lakini kwa upande mwingine wanastahili kulaumiwa na wazalendo wa lugha hii." Toa hoja nne (4) kutetea madai hayo.

2. Kwa kutoa mifano hai minne (4) eleza jinsi Kiswahili kama ilivyo kwa lugha yoyote kinavyokwenda na wakati.

3. "Shughuli zilizofanywa na Waarabu katika nchi za Afrika Mashariki zilikuza na kudumaza lugha ya Kiswahili". Toa hoja nne (4) kuthibitisha dai hilo.

## SEHEMU B (alama 20)

## SARUFI

4. Fafanua dhana ya uwakilishi katika sentensi kwa kutoa mifano minne (4) kudhihirisha maelezo yako.

5. Viambishi vijenzi katika lugha ni viambishi ambatishi na viambishi nyambuaji. Kwa kutumia mifano mitatu (3) kwa kila kiambishi eleza tofauti iliopo kati ya viambishi hivyo.

6. Ainisha sentensi zifuatazo na eleza sababu za mwainisho wako:

    (a) Ugonjwa wa UKIMWI hautibiki na wala kukingika.

    (b) Ulifika na paka wako pwani ili paka wako anyooshe mwili wake na kupunga hewa safi.

    (c) Lisemwalo lipo.

    (d) Akiniamkia nitamwitikia.

    (e) Kalamu haina wino.

## SEHEMU C (alama 20)

## MATUMIZI YA LUGHA

7. "Lugha ya mazungumzo hutawaliwa na mada ya mazungumzo, wahusika katika mazungumzo hayo, na mahali." Thibitisha usemi huo kwa kutumia mifano sita (6), yaani mifano miwili kwa kila kipengele.

8. "Mjuzi wa lugha zaidi ya moja, ujuzi wake hauwezi kuwa wa kiwango sawa." Fafanua sababu zinazoleta utofauti huo.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

9. Kwa kutumia mifano eleza maana, chanzo, aina na matumizi ya misimu katika Kiswahili.

## SEHEMU D (alama 20)

## UTUNGAJI

10. Andika barua gazetini kwa Mhariri wa gazeti la Nipashe ijumaa ya tarehe 18 Februari 2011, kumsifu mpokeaji simu wa Maktaba ya Taifa kwa huduma yake nzuri kwa wasomaji.

11. Andika insha ya maneno yasiyozidi mia nne (400) na yasiyopungua mia tatu (300) juu ya wanafunzi wengi kushindwa somo la Hisabati.

12. Kwa niaba ya wanafunzi wenzako wa Kidato cha Sita andika hotuba yenye maneno yasiyopungua mia tatu (300) ambayo itasomwa mbele ya mgeni rasmi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi, siku ya mahafali yenu.

## SEHEMU E (alama 20)

## UFAHAMU

13. Soma habari hii kisha jibu maswali yanayofuata:

Siku ya pili Mzee Tindo hakuwa kama kawaida yake. Hakuwasemesha wenzake kwa _bashasha_ kama ilivyo desturi yake. Alizungumza nao kikazi tu, na baada ya kumaliza aliondoka peke yake. Waliagana wakutane usiku Mlandege kwa safari ya kwa Morarji.

Wakati ulipofika wote walikutana pale walipoagana na walianza safari yao. Walipofika tu walilikuta lango kubwa la nyumba ya Morarji hapo Hurumzi liko wazi. Ukumbi wa jumba hilo ulikuwa uking'ara kwa mataa ya umeme yaliyoko katika kila ukuta wa kuta nne za ukumbi huo.

Morarji na mwenzake mmoja wa Kibaniani walikuwa wamekaa hapo ukumbini. Walikuwa wamekaa juu ya jukwaa lililotandikwa kwa mito iliyovishwa foronya nyeupe. Wote walikuwa _wamejitawanya_ juu ya mito hiyo ambayo ilikuwa laini kabisa. Walivaa mashati marefu ya _bafta_ yaliyokuwa na vifungo mpaka kooni. Walivaa pia _winda_ nyembamba ambazo hazikuweza kuwasitiri vizuri.

Mbele yake Morarji palikuwa na sanduku zuri la _msaji_. Morarji na mwenzake walikuwa wanazungumza Kibaniani. Mzee Tindo na wenzake walipofika mbele ya lango la nyumba hiyo walipata hofu kuingia ndani, lakini Rashidi bila ya kujali kitu chochote ndiye aliyekuwa wa mwanzo _kukifuka_ kizingiti cha lango hilo na kuingia ndani. Iliwabidi wenzake, yaani Farjalla na Mzee Tindo wamfuate, na wote kwa umoja wao waliingia ndani, na kukabiliana na Morarji uso kwa uso.

"Min nataka hapa" Morarji aliwauliza kwa sauti ya kijeuri.



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org

"*Mukki*!, si umesema tuje kukuona leo usiku?" Mzee Tindo alijibu huku hofu imemjaa. Morarji hata hakujali, aliendelea kuzungumza Kibaniani na mwenzake. Walizungumza kwa muda mrefu huku akina Rashidi na wenzake wakiwa wamesimama hapo mlangoni.

"Sasa nan nasema pesa hapana tosha? Wewe; wewe -------". Morarji aliuliza baada ya kuacha mazungumzo yake huku akimnyooshea kidole Rashidi na Farjalla ili kutaka kujua ni yupi hasa aliyesababisha matata. Farjalla alisimama kama hayupo, kimya kabisa, lakini Rashidi alijibu.

"Ndiyo Mukki pesa kidogo, hazitoshi". "Nan mwingine nasema pesa hapana tosha?" Morarji aliuliza tena.

Wote walinyamaza kimya wamenywea kama waliotiwa maji. Rashidi *mabega yalimpwaya* alipohisi wenzake *wamemtupa mkono*.

"Basi kama wewe nasema pesa haitoshi kwenda tafuta kazi pahali ingine iko pesa mingi!". Morarji alimwambia Rashidi kwa fedhuli, kisha alimgeukia Mzee Tindo na kumwambia, "Tindo, hapana chukua yeye kazini tena, haya! Jao!" Wote waliondoka na kuelekea makwao.

"Kujua kwingi huko, sasa unaona faida yake?" Mzee Tindo alisema huku akimfanyia *tashtiti* Rashidi. Rashidi hakujibu kitu alinyamaza kimya na kufuata njia yake moja kwa moja mpaka kwao.

**Maswali**

(a) Toa maana ya maneno yaliyopigiwa mstari katika habari hii.

(b) Mwandishi anatoa ujumbe gani kwa hadhira yake?

(c) Unafikiri ni kwanini Mzee Tindo hakuwa na bashasha kama ilivyokuwa desturi yake?

(d) Mwandishi anaposema "Wote walinyamaza kimya kama waliotiwa maji." Unapata taswira gani katika usemi huo?

(e) Kwa maoni yako unakionaje kitendo cha Rashidi kukaa kimya na kuelekea kwao baada ya kufanyiwa tashtiti na Mzee Tindo?



Find more free educational resources at http://maktaba.tetea.org